**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA**

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb. Na.KDC/L.50/9VOL.I/38** **Tarehe 04/08/2022**

## YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa anawatangazia nafasi za kazi Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zifuatazo:-

### 1.0 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – NAFASI 02

### 1.1 SIFA ZA MUOMBAJI:

Muombaji awe amehitimu kidato cha Nne na mwenye cheti cha utunzaji kumbukumbu (NTA Level 5) katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi.

### 1.2 KAZI NA MAJUKUMU.

i. Kutafuta kumbukumbu/ nyaraka/ majalada yanayohitajiwa na wasomaji.

ii. Kuthibiti upokeaji, Uandikishaji wa kumbukumbu /nyaraka.

**iii.** Kuchambua, kuboresha na kupanga kumbukumbu/ nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (classification and boxing) kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.

iv. Kuweka / kupanga kumbukumbu nyaraka katika reki (file racks/ cabinets) katika masijala / vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.

**v.** Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka n.k) katika majalada.

vi. Kushughulikia maombi ya kumbukumbu / nyaraka kutoka taasisi za Serikali.

### 1.3 MSHAHARA

Cheo cha Msaidizi wa kumbukumbu Daraja la II kina Ngazi ya **Mshahara wa TGS. B.**

**MASHARTI YA MAOMBI**

i) Muombaji awe raia wa Tanzania.

ii) Muombaji awe na umri kati ya miaka 18 na umri uslozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.

iii) Maombi yaambatanishwe na maelezo binafsi (CV), anwani sahihi na namba za simu.

iv) Maombi yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, cheti cha kidato cha nne, cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha NIDA na picha moja (01) ya passport size ya hivi karibuni.

v). Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 19/08/2022.

vi). Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa Anwani ifuatayo:-

12. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa Anwani ya:-

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa,**
**S.L.P 01,**
**KONDOA.**

Rahiya Nasser
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**KONDOA**

MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA
KONDOA

**Nakala:**

Katibu wa Tume,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320,
**DODOMA.**

**Tovuti ya Halmashauri**
**www.kondoadc.go.tz**

**Mbao za matangazo**